



## MSAADAA KWA WATU WAZIMA

SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI  
KWA AJILI YA WAATHIRIKA WA  
USA FIRISHAJI WA BINADAMU

Mwombe mtoto asome Yohana 10:10: "...mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele."

### WASHIRIKISHE SEHEMU HII KWA NJIA YA UBUNIFU

Biblia ina hadithi nyingi juu ya Mungu anavyotupenda kila mmoja hapa duniani. Yesu alihadithia hadithi juu ya mkulima na kondoo wake.

Palikuwepo mkulima mzuri, aliywapenda kondoo wake. Alifanya kazi kwa bidii sana ili kuhakikisha wote walikuwa na afya na usalama. Kila siku mkulima aliwahesabu kondoo wake ili kuhakikisha hata mmoja hapotei. (Unaweza kuwahesabu watoto) 1, 2, 3, 4...99, 100! ...1,2,3,4,99,100. 1,2,3,4,99,100. Lakini siku moja, palijitokeza hitilafu. 1,2,3,4,99...99...99 – Hapana! Palikuwa na kondoo 99 peke yake! Mmoja wa kondoo wa thamani wa mkulima alikuwa hayupo! Mkulima alijichukulia chakula cha njiani akaondoka kwenda kumtafuta kondoo aliyejkuwa haonekani. Alijua hawesi kurudi nyumbani mpaka ampare huyo kondoo kwani kila kondoo wake alikuwa kondoo wa thamani sana. Aliwapenda sana kondoo wake. Hakutaka hata kondoo mmoja aukose uzima kamili. Alipanda milima (unaweza kuigiza unapanda mlima), aliogelea kwenye maji (unaweza kuigiza unaogelea) na mwishowe, alimpata kondoo aliyepotea! Alikuwa na furaha sana! Akampeleka kondoo mpaka nyumbani. 1,2,3,4,99,100! Mkulima aliwapenda kondoo wake wote. Naye alikuwa tayari kufanya lolote kuhakikisha kondoo wake wako salama, wana afya njema na wanaweza kuishi maisha makamilifu.

### MASWALI YA MSHANGAO

Sijui ni sehemu gani ya hadithi hii uliyoipenda zaidi? Sijui ni sehemu gani ya hadithi hii iliyokukumbusha juu ya Yesu?

Sijui ni sehemu gani ya hadithi inakuhusu wewe?  
Sijui inamaanisha nini kuwa na maisha makamilifu?

Utumwa na usafirishaji ni mambo mabaya. Ni wakati ambao watu hunyang'anywa uhuru wao, na kulazimishwa kufanya kazi katika njia mbazo huwaacha wakiwa sio salama nao hutendewa kama wasio na thamani. Huwa hawawezi kuishi maisha makamilifu tena. Watu wakitendewa vibaya namna hii, humpa Mungu masikitiko makubwa na hata humkasirisha. Mungu hapendi hata mmoja wa watu wake wa thamani ahuzunishwe, aumizwe na awe mpweke. Mungu anataka kila mmoja ayapate maisha makamilifu. Anasema anaweza kuwasaidia watu wanaotendewa vibaya. Tunaweza kusaidia kueneza habari yake njema ya heshima, ya upole na upendo kwa watu wote duniani, ili watu watendeane vema. Tunaweza kusaidia vile vile kwa kuwaomba viongozi wawalinde watu vizuri zaidi, ili wasiumizwe na wengine. Humpendeza Mungu sana kujua kwamba ana watoto wanaomsaidia kusambaza upendo na kuifanya dunia iwe mahali salama zaidi.

### WAFUNDISHE WATOTO

**Siri haziko salama** – Wakati fulani tunaweza kuwapa watu mshangao; tunaweza kumnunulua mtu zawadi ambayo hakutarajia kuipata. Lakini kitu cha mshangao na kitu cha siri ni vitu viwili tofauti. Watoto wetu wakubwa na watu wazima wanao tupenda hawawezi kutuomba tutunze siri. Kama mtu akikuomba ufiche kitu, unaruhusiwa kumwambia mtu mzima unayemwamini. Kama mtu akikwambia utunze siri kati yako na yeye, unaweza kumwambia mtu mzima unayemwamini.

**Mungu alikuumba ukiwa wa thamani** – Waulize watoto, kitu cha thamani sana kwako ni kipi? Kitu kikiwa cha thamani, tunakitendeaje? Ulifahamu kwamba Mungu alikuumba ukiwa wa thamani? Mikono yako, miguu yako, akili zako, hisia zako – kila sehemu ya mwili wako ni ya thamani! Mungu anataka kila mmoja amtendee mwenzie kama mtu mwenye thamani. Kwa huzuni, wakati fulani watu hawafanyi hivi. Kama mtu akikutendea mabaya, unaruhusiwa kumwambia hapana. Unaweza vile vile ukamwambia mtu mzima unayemwamini.

### SHUGHULI

#### Siri dhidi ya mishangazo!

Panga upande mmoja wa chumba uwe "siri" na upande wa pili uwe "mishangazo". Waambie watoto watafanya maigizo. Watatakiwa kukimbilia upande wanaoona ni sahihi kama ni siri au ni mshangazo. Swala litabadilika kulingana na unavyoona ni sahihi. Hapa chini pana mifano michache:

- Rafiki anasema patakuwa na sherehe ya kuzaliwa, na haambivi mvulana/msichana anayehusika (mshangazo)
- Mwana familia usiyemjua vizuri sana anasema anaweza kukununulua zawadi, lakini usimwambie mama au baba (siri)

#### Mimi ni wa thamani! (mchezo wa kukumbuka)

Watake watoto wakae katika duara. Watapeana zamu kuzunguka duara, wakitaja jambo moja linalowafanya wenyewe thamani. Zamu ya mmoja ikifika, ataje jibu lake, na kisha warudie jibu la kila mmoja katika duara ambaye amekwisha kutoa jibu lake.

#### Sema kwa sauti!

Waruhusu watoto kufanya mazoezi ya kuzungumza kwa sauti kwa mzaha. Tumia misemo kama "sijisikii niko salama", "sitaki", "Hilo hunifanya nijisikie vibaya". Wafanye watoto watengeneze tendo, na waseme kwa sauti pamoja msemo waliochagua. Wape matukio rahisi na waseme ule msemo kwako, kama:  
'Njoo nami, familia yako haitajali.' – 'Sijisikii niko salama'  
'Chukua hiki kimoja, itakuwa sio vibaya' – 'Sijisikii niko salama'